


PROGRAMU YA KUFUNDISHA KIINGEREZA KWENYE SHULE YA MAPLEWOOD.

Kuhudumia Wanafunzi wa lugha nyingi katika muundo unaojumuisha na jumuishi

KUFUNDISHA VIWANGO VYA LUGHA NA HESABU

Wanafunzi kwenye programu ya EL wanasomeshwa madarasa za hesabu na sanaa, hizi zinafundishwa na mwalimu wa hilo darasa na anasaidiwa na mwalimu wa kingereza.



MAENDELEO YA LUGHA YA KIINGEREZA

Wanafunzi huondoka kwenye Programu ya EL baada ya kupata kiwango cha 5 kwenye Jaribio la ACCESS, ambalo hupima lugha ya kitaaluma ya kiingereza. Maendeleo ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wetu inatokea kwa kufundishwa na walimu wawili, Programu ya TWI na kwa Darasa la Maendeleo ya Lugha ya Kiingereza haswa kwa wanafunzi wapya inchini.

WASIMAMIZI WA KESI ZA EL

Wanafunzi kwenye Programu ya EL huwa na walimu wenye kuhudumia kesi zao. Wasimamizi wa kesi hufanya kazi na mwanafunzi, walimu wa mwanafunzi na familia ya mwanafunzi kwa kusaidiana kuelewa maendeleo ya lugha na mahitaji zingine za mwanafunzi kwa kumusaidia aweze kufaulu shuleni.



PROGRAMU YA KUFUNDISHA KWA NJIA YA LUGHA MBILI

Kupitia darasa zetu zilizofundishwa, sisi tunatoa mipango ya lugha mbili kwa kukuza lugha ya masomo ya wanafunzi kwa kusoma na kuandika katika Kihispania na kiingereza. Madarasa hzinafundishwa kwa hesabu, masomo za kijamii na Lugha ya Ulimwengu ya Uhispania.

